JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Simu ya mdomo: 255 22 2460735/2460706-8
FAKSI: 255 22 2460 735/700
Simu pepe: met@meteo.go.tz
Tovuti: www.meteo.go.tz

S.L.P. 3056
DAR ES SALAAM

Unapojibu tafadhali nakili:

Kumb. Na.: TMA/1622

05 Januari, 2017

TATHIMINI YA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA OKTOBA – DISEMBA 2016

Taarifa hii inatoa tathimini ya mvua za msimu wa Vuli (Oktoba-Disemba) kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Vile vile taarifa hii inatoa uchambuzi wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua kwa kipindi cha Novemba 2016 hadi Februari, 2017 kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka.

A: MUHTASARI

i. TATHIMINI YA MVUA ZA VULI (OKTOBA HADI DISEMBA, 2016)

Tathimini ya mvua za Vuli katika kipindi cha miezi ya Oktoba - Disemba, 2016 katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka inaonesha kuwa kwa ujumla maeneo mengi mvua zimenyesha katika kiwango cha chini ya wastani na mtawanyiko usioridhisha. Katika kipindi cha miezi ya Oktoba hadi Disemba 2016 maeneo mengi ya Ukanda wa Ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mwanza na Mara) mvua zimenyesha kwa kiwango cha wastani hadi chini ya wastani. Maeneo mengi ya nyanda za juu kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara) mvua zimenyesha katika kwango cha chini ya wastani. Mvua za chini ya wastani zimenyesha pia katika maeneo ya ukanda wa Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Visiwa vya Unguja na Pemba).



Kielelezo1.1: Mvua zilivyonyesha kwa maeneo yanayopata mvua za vuli

ii. TATHIMINI YA MVUA ZA MSIMU

Mvua za msimu kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka Mikoa ya Kigoma Tabora Katavi, Singida Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma, Lindi na Mtwara zinaendelea kunyesha na zinatarajiwa kuisha mwishoni mwa mwezi Aprili, 2017.

iii. MATUKIO

Katika kipindi cha msimu wa mvua kwa miezi ya Oktoba hadi Disemba, 2016, kumekuwa na matukio ya vipindi vya mvua kubwa, upepo mkali, radi na mvua ya mawe katika baadhi ya maeneo hapa nchini. Matukio hayo yamesababisha uharibifu wa mali, makazi na miundombinu. Baadhi ya matukio ya mvua kubwa yaliojitokeza katika baadhi ya meneo kama ifuatavyo; tarehe 14/12/2016 milimita 108.5 katika kituo cha Naliendele (Mtwara), tarehe 31/12/2016 milimita 94.4 katika kituo cha Mlingano (Tanga) na tarehe 18/11/2016 milimita 61.4 katika kituo cha hali ya Hewa Kigoma (Kigoma).

B: MWELEKEO WA MIFUMO YA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI FEBRUARI, 2017

Katika kipindi cha mwezi Januari na Februari, 2017 hali ya joto la bahari katika ukanda wa tropikali ya mashariki mwa bahari ya Pasifiki inatarajiwa kuwa chini ya wastani ambapo hali ya joto la baharí katika eneo la kusini magharibi mwa baharí ya Hindi inatarajiwa kuongezeka. Mgandamizo mkubwa wa hewa kutoka Siberia unatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali ya joto la bahari katika bahari ya Atlantiki eneo la karibu na

pwani ya Angola linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha msukumo wa hewa yenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo pia kusababisha makutano ya upepo katika maeneo ya magharibi, kusini magharibi na kati mwa nchi.

C: MVUA ZA VULI (OKTOBA –DISEMBA).

Katika kipindi cha mvua za msimu wa Vuli maeneo mengi yalipata mvua za chini ya wastani. Hata hivyo baadhi ya maeneo yamepata mvua za nje ya msimu.

D: MWELEKEO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI HADI FEBRUARI, 2017

Mvua za Msimu

Kipindi cha mvua za Msimu kilichoanza mwezi Novemba, 2016 kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (Mikoa ya Kigoma Tabora Katavi, Singida Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma, Lindi na Mtwara) kinatarajiwa kuendelea hadi Aprili, 2017.

Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani katika maeneo mengi. Hata hivyo maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Lindi yanatarajiwa kupata mvua chini ya wastani katika kipindi cha mwezi Januari hadi Februari, 2017.

Kanda ya Magharibi (Mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma):
Mvua zinaendelea kunyesha na zinatarajiwa kuwa za wastani katika kipindi cha mwezi Januari na Februari, 2017.

Kanda ya kati (Mikoa ya Singida na Dodoma):
Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika kipindi cha mwezi Januari na Februari, 2017.

Nyanda za juu Kusini Magharibi: (Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro:
Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuendelea kunyesha katika kiwango cha wastani katika kipindi cha mwezi Januari na Februari, 2017 .

Kanda ya kusini na Pwani ya kusini (Mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi):
Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani, hususan mikoa ya Ruvuma, Mtwara pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Lindi katika kipindi cha mwezi Januari na Februari, 2017.

Mamlaka ya Hali ya Hewa inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

KUMB: *Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi miwili) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia tabiri za saa 24, siku 10 pamoja na za mwezi kama zinavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.*

IMETEOLEWA NA MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA